# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS
# MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

## MWONGOZO WA MAVAZI KWA WATUMISHI WA UMMA

KWA MUJIBU WA WARAKA WA UTUMISHI WA UMMA NA. 6 WA MWAKA 2020

## MAVAZI YANAYORUHUSIWA NA YASIYORUHUSIWA, MATUMIZI NA VIWANGO VYA UNADHIFU KWA WATUMISHI WA UMMA

## A: MAVAZI YANAYORUHUSIWA NA VIWANGO VYA UNADHIFU



### KIWANGO CHA KAWAIDA (CASUAL)

(a) Gauni na au hijabu;
(b) Blauzi na sketi/suruali na au hijabu;
(c) Siku ya Ijumaa au siku yoyote itakayoamuliwa na Mwajiri na au siku za maadhimisho, ivaliwe blauzi ya kitenge blauzi/fulana yenye kola yenye maudhui ya kitaasisi na sketi au suruali na au hijabu kwa watumishi wa ngazi zote.



### KIWANGO CHA KATI (CASUAL SMART)

(a) Gauni na koti au blauzi yenye mikono mirefu au mifupi na au hijabu;
(b) Sketi/suruali na blauzi/ koti na au hijabu;
(c) Vazi la kitenge na au hijabu.



### KIWANGO CHA JUU (SMART)

(a) Suti ya sketi/suruali na au hijabu;
(b) Blauzi na sketi/suruali na au hijabu;
(c) Vazi la kitenge na au hijabu.



### KIWANGO CHA KAWAIDA (CASUAL)

(a) Suruali na shati;
(b) Suruali na shati na au sweta;
(c) Siku ya Ijumaa au siku yoyote itakayoamuliwa na Mwajiri na au siku za maadhimisho, ivaliwe shati la kitenge/fulana yenye kola yenye maudhui ya kitaasisi na suruali kwa watumishi wa ngazi zote au kanzu na koti pamoja na barkashia.



### KIWANGO CHA KATI (CASUAL SMART)

(a) Suruali na shati la kitenge;
(b) Suruali na shati pamoja na tai na au sweta;
(c) Suruali na shati pamoja na koti bila tai;
(d) Kaunda/safari suti ya mikono mifupi.



### KIWANGO CHA JUU (SMART)

(a) Suti ya kimagharibi na tai;
(b) Kaunda/safari suti ya mikono mirefu yenye kola au isiyo na kola;
(c) Suruali na shati la kitenge.

## MAHALI NA MATUMIZI YA VIWANGO VYA UNADHIFU

### MAVAZI YA KAZI ZA KAWAIDA ZA OFISI

ANAWEZA KUVAA MAVAZI YA
(a) Kiwango cha kawaida;
(b) Kiwango cha kati;
(c) Kiwango cha juu.

### MAVAZI KWENYE MIKUTANO YA OFISI AU TAASISI

ANAWEZA KUVAA MAVAZI YA
(a) Kiwango cha kati;
(b) Kiwango cha Juu.

### MIKUTANO BAINA YA TAASISI, YA KITAIFA AU KIMATAIFA

MTUMISHI AVAE MAVAZI
(a) Kiwango cha Juu.

### MAVAZI MENGINEYO

(a) Mavazi kwenye kazi maalum
Zivaliwe nguo maalum za utekelezaji wa kazi husika. (Mfano; Madaktari, Wahandisi, Michezo n.k)
(b) Safarini, Sikukuu/siku za mapumziko
Mtumishi atavaa "free casual".

## B: MAVAZI NA MUONEKANO USIORUHUSIWA KWA MTUMISHI WA UMMA MAHALI PA KAZI



Jinzi

"MTUMISHI WA UMMA ANAPASWA KUZINGATIA WARAKA HUU MUDA WOTE AWAPO KAZINI"

(a) Nguo za kubana au kuonyesha maungo ya mwili;
(b) Nguo za kuacha wazi sehemu ya juu ya magoti, kitovu, kifua, mgongo, mabega, khanga na madera;
(c) Nguo zenye maandishi/alama ya chama chochote cha siasa, picha, michoro na maandishi yasiyoendana na kazi za serikali;
(d) Nguo zinazoangaza mwili (Transparent) na zinazo meremeta;
(e) Suruali fupi (pedo), kaptula, nguo aina ya jinzi na suruali zenye mifuko mingi;
(f) Viatu vya rangi mchanganyiko (Me) na viatu vya wazi;
(g) Viatu virefu (High heels) zaidi ya inchi tano kwa wanawake;
(h) Uvaaji mikufu juu ya nguo kwa wanaume;
(i) Nywele na ndevu zenye rangi kali (bleach);
(j) Kucha zaidi ya mm 5 na zenye mchanganyiko wa rangi;
(k) Uvaaji wa suruali mlegezo;
(l) Michoro ya kudumu (Tatoo) sehemu za wazi za mwili;
(m) Uvaaji wa hereni na kusuka nywele kwa wanaume.